



Ukuzaji na Uenezaji wa Lugha ya Kiswahili katika Karne ya 21 Kupitia Maazimio, Matamko na Ushauri wa Viongozi wa Serikali katika MASIKIDU

Editha Adolph

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Tanzania

Uwasilishaji wa Makala

Pokelewa: 2023-01-02

Rekebishwa: 2023-04-14

Kubalika 2023-05-18

Chapishwa 2023-05-20

Maneno Muhimu

MASIKIDU

Ukuzaji

Kiswahili

Ushauri

Jinsi ya Kurejelea Makala

Adolph, E., (2023). Ukuzaji na Uenezaji wa Lugha ya Kiswahili katika Karne ya 21 Kupitia Maazimio, Matamko na Ushauri wa Viongozi wa Serikali katika MASIKIDU. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 1(1), 31-46.

Copyright © 2023



Ikisiri

Makala hii inachunguza ukuzaji na uenezaji wa lugha ya Kiswahili katika karne ya 21 kupitia maazimio, matamko fursa na ushauri wa serikali kabla¹ na wakati wa MASIKIDU (siku ya maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani). Azma kuu ni kuangazia namna maazimio, fursa, ushauri na matamko mbalimbali yaliyotolewa na viongozi wa serikali katika MASIKIDU yanavyolenga kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili. Ili kutimiza azma hii, mtafiti ametumia hotuba ya Mh. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais wa Tanzania Mh. Philip Mpango, Mh. Mohamed Mchengerwa waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mh. Adolph Mkenda Waziri wa Elimu nchini Tanzania na ya Mh. Abdulrahman Kinana makamu mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara kama marejeleo ya maazimio, matamko, fursa na ushauri huo. Kimsingi utafiti huu ni wa uwandani. Utafiti huu umetekelezwa kwa mujibu wa mkabala wa maelezo. Mtafiti alikusanya data kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji. Matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa viongozi mbalimbali wa Tanzania wametoa maazimio mbalimbali kuhusiana na lugha ya Kiswahili kupitia MASIKIDU. Miongoni mwa maazimio hayo ni: uanzishwaji wa vituo vya kufundishia Kiswahili kwa

¹ Ikimbukwe kuwa maadhimisho haya yalifanyika kwa juma zima. Hivyo, kuna maazimio, ushauri na matamko yaliyotolewa siku moja kabla ya maadhimisho hayo. Mathalani, maazimio, ushauri na matamko ya Mh. Abdulrahman Kinana na Mh. Mohamed Mchengerwa yalitolewa tarehe 06 Julai, 2022.



wageni, kutoa mafunzo kwa wataalamu wa nyanja mbalimbali za Kiswahili, serikali kutekeleza mkakati wa taifa wa kukifanya Kiswahili kijiuze, ushawishi wa nchi nyingine kuingiza Kiswahili katika mitaala yao.. Aidha, viongozi wameelekeza matumizi ya Kiswahili katika nyaraka za mawasiliano za wizara na idara zake, mikutano, warsha, semina, mijadala ya umma na dhifa, majina ya barabara, mitaa, mabango, fomu za usaili na maelekezo ya matumizi ya dawa zote na bidhaa. Makala hii ni muafaka kwa wazungumzaji na wanaojifunza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania kwani inahamasisha juu ya uandishi, tafsiri, ufundishaji na ujifunzaji wa lugha hii sambamba na fursa lukuki zanzotokana nayo. Vilevile inaonesha ni kwa jinsi gani viongozi wa Tanzania walivyo na mapenzi mema kwa lugha hii aushi na adhimu ya Kiswahili ambapo hii ni chachu ya kukua na kuenea lwa lugha hii. Mtafiti anapendekeza tafiti fuatizi zifanyike juu ya maazimio, matamko fursa na ushauri unaotolewa na viongozi mbalimbali kuhusiana na lugha ya Kiswahili sambamba na utekelezaji wake.

Utangulizi

Kiswahili ni miongoni mwa lugha kumi zinazozungumzwa zaidi duniani na inakadiriwa kuwa lugha hii ina wazungumzaji zaidi ya milioni mia mbili. Mbali na kwamba lugha hii inazungumzwa nchini Tanzania, pia huzungumzwa katika nchi nyingine kama vile: Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Sudan Kusini, Somaria, Malawi, Zambia, Msumbiji, Komoro, Boman na Yemen (Mulokozi, 1992). Kuenea na kutumika kwa lugha ya Kiswahili kumezungumziwa kupitia wataalamu mbalimbali mathalani, Shariff (1988), Mazrui na Alamin (1998), Mazrui na Shariff (1994), Gibbe (1983), Massamba (2007), Mutembe (2011) na Mutembe (2016). Kwa mujibu wa Msanjila (2005) ni kwamba lugha hii imevuka mipaka ya nchi zake asilia: Tanzania na Kenya na kuenea karibia kwenye nchi zote Afrika Mashariki na Kati. Kiswahili kimeenea katika nchi hizi kwa viwango tofauti. Anaongeza kwa kusema kuwa, katika nchi hizi, hakuna lugha nyingine ya Kiafrika iliyo na sifa ilizonazo lugha hii ya Kiswahili. Aidha, Kimathi na Mukuthuria (2017) wanafafanua kuwa Kiswahili kina hadhi ya lugha rasmi na lugha ya taifa katika nchi ya Kenya na Tanzania: hadhi ya lugha rasmi nchini Uganda na Rwanda; na kisera, ni lugha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Wataalamu mbalimbali mathalani, Mwansoko (2016) wamechunguza masuala kadhaa yanayokikua Kiswahili. Miongoni mwa masuala mengine, Mwansoko anasema kuwa tafsiri imetoa mchango mkubwa katika ukuzaji na ustawishaji wa lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa mambo mengine, amebainisha baadhi ya manufaa ya tafsiri kwa Kiswahili kama ifuatavyo: mosi, kukitangaza Kiswahili kimataifa. Kutokana na sababu hii Kiswahili kimetambulika ulimwenguni na kuwa miongoni mwa



lugha kubwa na muhimu ulimwenguni. Hii ni kutokana na sababu kuwa lugha nyingi mathalani Kiingereza, Kikorea, Kichina, Kifaransa, Kirusi nakadhalika, zimekuwa zikitafsiriwa katika Kiswahili na kukifanya Kiswahili kutambulika pia katika jamii za kigeni zinazotumia lugha hizo. Mtaalamu huyu anaendelea kusema kuwa, mfano halisi wa hayo yaliyofafanuliwa hapo juu ni uthubutu wa Mwl. J. K. Nyerere wa kutafsiri katika Kiswahili tamthiliya mbili za mwandishi mashuhuri wa Uingereza wa karne ya 16, William Shakespeare ambazo ni Julius Caesar na *The Merchants of Venice*. Pili, ni kukuza msamiati na istilahi za Kiswahili. Tafsiri mbali na kukitangaza Kiswahili kimataifa, pia ni chanzo kikubwa cha kukuza msamiati na istilahi za Kiswahili. Kwa mfano, kupitia tafsiri zimeandaliwa istilahi na msamiati wa masomo na taaluma mbalimbali. Baadhi ya msamiati na istilahi hizo ni kama hizi zifuatazo:

Kiingereza	Kiswahili
Pythagoras	Paithagorasi
Frankfurt	Frankifuti
Tripolis	Tripoli
Askari jera	Jela gaoler

Chanzo: Mwansoko (2016)

Tatu, uingizaji wa miundo mipya ya misemo katika Kiswahili. Lugha ya Kiswahili imeendelezwa na kukuzwa na tafsiri kwa kuingiziwa miundo mipya ya misemo. Hii ni kutokana na sababu kuwa tafsiri ya kisemantiki huegemea zaidi upande wa mwandishi wa matini chanzi na kutaka kufasiri kila kipashio katika matini hiyo. Tuone mifano anayotoa mtaalamu huyu katika kuthibitisha hoja hiyo:

Kiingereza	Kiswahili
May I take this opportunity to...	naomba nichukue fursa hii ku....
Ladies and gentlemen	mabibi na mabwana
Honourable Speaker	mheshimiwa Spika
It was resolved that	iliazimiwa kuwa

Chanzo: Mwansoko (2016)

Nne, kukuza fasihi ya Kiswahili. Kiwango cha fasihi ya Kiswahili hupanuliwa kutokana na tafsiri za maandiko ya kifasihi kutoka lugha zilizoendelea, hasa za waandishi mashuhuri. Mwansoko (2016) anafafanua kuwa maandiko hayo aghalabu huwakilisha matokeo ya urithi wa vizazi na vizazi, na mara nyingine hata kwa zaidi ya karne. Utajiri wa fasihi hizo huchangia katika makuzi ya fasihi ya Kiswahili. Tofauti na utafiti wa Mwansoko (2016) uliochunguza ukuzaji wa Kiswahili kupitia tafsiri, utafiti wa sasa unaangazia ni kwa namna gani maazimio, matamko na ushauri uliotolewa na viongozi mbalimbali kwenye MASIKIDU unalenga kukukuza na kukieneza Kiswahili duniani katika karne ya 21.

Mbali na Mwansoko (2016) aliyeangalia ukuzaji na uenezaji wa lugha ya Kiswahili kupitia tafsiri, Hans (2016) kupitia andiko lake la kutathmini utekelezaji wa matamko ya viongozi waandamizi wa serikali ya Tanzania kuhusu matumizi ya Kiswahili, ameonesha masuala kadhaa yanayokuza na kuendeleza lugha adhimu na aushi ya Kiswahili. Miongoni mwa mambo hayo ni; viongozi wa serikali kutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zao za kiserikali, mikutano mbalimbali ya hadhara ikiwa



ni pamoja na mikutano ya kampeni za kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kufanyika kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hii imewasaidia wananchi wengi kuelewa kinachoendelea katika nchi yao. Masuala mengine aliyoyabainisha mtaalamu huyu ni suala la raisi wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujiwekea utaratibu wa kutoa hotuba kila mwisho wa mwezi kwa lugha ya Kiswahili, barua na nyaraka nyingi za serikali kuandaliwa kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa wabunge na mawaziri wengi kupitia vipindi vya bunge vinavyorushwa na vyombo mbalimbali vya habari, hujitahidi sana kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na wakati wa kutoa hotuba licha ya kanuni za bunge kuwaruhusu kutumia hata lugha ya Kiingereza. Anathibitisha hoja hii kwa kusema kuwa, 'binafsi sijawahi kumsikia mbunge au waziri akitoa hotuba yake kwa lugha ya Kiingereza, ingawa kanuni za bunge zinawaruhusu kufanya hivyo'. Anamalizia kwa kusema kuwa mambo yote haya na mengine mengi hukifanya Kiswahili kikue na kuenea kwa kasi na kulifanya taifa letu kuwa mfano wa kuigwa katika matumizi ya Kiswahili duniani. Utafiti wa Hans (2016) ni muhimu katika makala hii kwani umedadavua kikamilifu namna matamko ya viongozi waandamizi wa serikali ya Tanzania ulivyotoa mchango mkubwa katika suala zima la kukieneza na kukikuza Kiswahili. Hii imetusaidia kujua ya kwamba pamoja na matamko na maazimio ya viongozi hao yanayoendelea kutolewa yalishashatangukiwa na mengine kabla. Utafiti wa Hans (2016) umejikita katika kutathmini utekelezaji wa matamko ya viongozi waandamizi wa serikali ya Tanzania kuhusu matumizi ya Kiswahili miaka ya 2016, makala yetu inachunguza maazimio ya serikali kuhusu Kiswahili na maendeleo yake katika karne ya 21 kwa kuangazia maazimio mbalimbali yaliyotolewa na viongozi mbalimbali wa serikali katika siku ya maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani 07/07/2022 (MASIKIDU).

MASIKIDU

MASIKIDU ni kifupisho cha maneno: Maadhimisho ya siku ya Kiswahili Duniani. Hii ni siku maalumu iliyoteuliwa kufuatia maamuzi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa ajili ya kuadhimisha na kukienzi Kiswahili duniani kote. Rasmi UNESCO ilipitisha azimio maalumu kupitia mkutano wake wa 41 huko Ufaransa mjini Paris November 23, 2021 na kuitangaza siku maalumu ya maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani kuwa ni 07/07 kila mwaka. Uamuzi huu ulifanyika kutokana na ufasaha, ukubwa na kuenea kwa lugha hii adhimu na aushi ya Kiswahili. Kwa mara ya kwanza maadhimisho haya yalifanyika 07/07/2022 hapa Tanzania na kwingineko duniani. Ifahamike kuwa Kiswahili ni lugha ya kwanza Afrika kupitishwa na UNESCO na kupewa siku maalumu ya kuadhimishwa duniani kila mwaka. Aidha, Kiswahili ni lugha ya nane duniani kupewa hadhi hii. Lugha nyingine zilizopewa hadhi ya kuadhimishwa kila mwaka ni pamoja na Kifaransa, tarehe 20 Machi, Kichina, tarehe 20 Aprili, Kiingereza, tarehe 23 Aprili, Kireno, tarehe 05 Mei, Kirusi, tarehe 06 Juni na Kiarabu, tarehe 18 Disemba.

Ukuzaji na Uenezaji wa Kiswahili katika Karne ya 21 Kupitia Maazimio, Matamko na Ushauri wa Viongozi wa Serikali katika MASIKIDU

Kama ilivyodokezwa awali kuwa Kiswahili kimeheshimishwa kwa kupewa siku yake maalumu ya kuadhimishwa duniani. Kwa mara ya kwanza maadhimisho hayo yamefanyika 07 Julai, 2022 na kuhudhuriwa na watu mbalimbali wakiwemo viongozi wa serikali. Aidha, shughuli kadhaa



zilifanyika ikiwa ni pamoja na matembezi, maonesho ya utamaduni wa Mswahili, michezo mbalimbali mathalani ngoma, uwasilishaji wa makala nakadhalika. Aidha, katika maadhimisho hayo yalitolewa maazimio, matamko na ushauri kutoka kwa viongozi mbalimbali wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hapa chini ni maazimio, matamko na ushauri huo:

Maazimio na Matamko ya Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Samia Suluhu Hassan

Awali ya yote tunakupongeza Mh. Raisi Dkt. Samia Suluhu Hassan wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutenga muda wako kwa ajili ya MASIKIDU. Aidha, tunakushukuru kwa maazimio na matamko yako yenye baraka tele na yenye raghba ya kukikuza, kukiendeleza na kukieneza Kiswahili duniani kote sambamba na kuwapatia watanzania fursa mbalimbali zinazotokana na lugha hii aushi na adhimu ya Kiswahili. Kama haitoshi, umeona ni vema kuwashirikisha viongozi wengine wa serikali jambo hili, hakika unaonesha ni kwa namna gani una mapenzi na malengo muhimu juu ya lugha hii ya Kiswahili. Hii inadhihirisha kuwa wewe ni miongoni mwa watu walio tayari kukienzi Kiswahili. Aidha, tunakushukuru kwa maazimio n matamko yako kuhusiana na lugha hii ya Kiswahili. Baada ya shukrani hizo yafuatayo ni maazimio na matamko ya Mh. Raisi Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa katika MASIKIDU. Baada ya ukaribisho kwa wageni na viongozi mbalimbali wakiwemo maraisi wastaafu, mabalozi wastaafu, viongozi wa chama na serikali, Mh. Raisi Dkt. Samia Suluhu Hassan aliwashukuru na kuwapongeza kwa mchango wao katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili duniani. Alieleza kuwa azimio la kuteuliwa Kiswahili kuwa lugha rasmi ya kazi katika umoja wa Afrika lilipitishwa katika mkutano uliofanyika huko Durban Afrika Kusini 09-11 July, 2002. Mh. Raisi alimshukuru Olusegun Obasanjo kwa hatua ya uthubutu kuhutubia mkutano wa wakuu wa nchi na serikali za umoja wa Afrika kwa Kiswahili wakati akifunga mkutano alipomaliza muda wake kwa kuwa mwenyekiti wa umoja wa Afrika Julai 2004. Aliongeza kwa kusema kuwa jambo hilo lilizaa mbegu iliyoendelea kukisambaza Kiswahili kikanda hadi kimataifa.

Aidha, alilishukuru Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni UNESCO kwa kutenga siku ya tar 07 July kila mwaka kuwa siku ya Kiswahili duniani na kusema kuwa kwa hakika imeipa lugha yetu ya Kiswahili heshima na hadhi kubwa. Aliongeza kuwa Tanzania ni chimbuko la lugha ya Kiswahili, hivyo, ni muhimu kukuza na kuendeleza lugha hii ndani na nje ya nchi. Aidha, alisema kuwa miongoni mwa mikakati ya serikali katika kukuza na kueneza Kiswahili ni pamoja na kuziwezesha ofisi za kbalozi zilizo nje ya Tanzania kuhamasisha uanzishwaji wa vituo vya kufundishia Kiswahili kwa wageni ambavyo walimu wake watakuwa ni vijana waliohitimu katika vyuo vyetu vikuu. Kuwawezesha watanzania watakojijuhusisha na taaluma za ukarimani, uhariri, tafsiri, ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni, utangazaji na uandishi wa Kiswahili kwa kuwapa mafunzo, kuwapiga msasa na kuwapatia nyenzo zitakazowapatia mbinu za kutekeleza kazi hiyo kwa ufanisi. Vilevile serikali itatekeleza mkakati wa taifa wa kukifanya Kiswahili kijiuze. Mh. Raisi aliendelea kufafanua kuwa uzinduzi huu utaongeza nguvukazi, miundombinu na bajeti kwa mabaraza, taasisi na vyuo vinavyofundisha Kiswahili ili viendeele kuandaa wataalamu zaidi watakaotumika duniani kote. Alimalizia kwa kusema kuwa mbali na maadhimisho haya ya kwanza ya siku ya Kiswahili duniani, nchi na balozi zake zitaendelea kuadhimisha siku ya Kiswahili duniani mwaka hadi mwaka. Ni faraja kwetu kuwa na mataifa mengine, taasisi na vyuo vikuu duniani navyo



vimeenzi maadhimisho haya, haya yalikuwa matamko na maazimio ya Mh. Samia Suluu Hassan raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Matamko na maazimio haya yanaonesha dhahiri kuwa Mh. Raisi ana mapenzi ya dhiti na nia njema juu ya Kiswahili. Halikadhalika, yuko tayari kuungana na watu wote wenye nia ya dhiti ya kukiendeleza Kiswahili duniani kote sambamba na kutoa mchango wa hali na mali kwa watazania watakaojitokeza kukieneza, kukiendeleza, kukikuzi na kukiuzu Kiswahili kupitia tafsiri, utangazaji, uandishi wa Kiswahili ukarimani, uhariri, ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni, nakadhalika. Baada ya kuona maazimio na matamko ya Mh. Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluu Hassan, tuone ni kwa namna gani viongozi wengine wanamuunga mkono na kushikamana naye katika suala zima la kukuza, kueneza na kuendeleza lugha ya Kiswahili.

Maazimio, Matamko na Ushauri wa Makamu wa Rais wa Tanzania Mh. Philip Mpango

Tunakupongeza Mh. makamu wa raisi wa awamu ya sita Philip Mpango kwa kusitisha shughuli zako na kuitikia wito wa kuwa mgeni rasmi katika siku hii muhimu ya kuadhimisha Kiswahili duniani. Umeonesha ni kwa namna gani una utayari wa kushirikiana na viongozi wengine hususan Mh. Raisi katika kuhakikisha Kiswahili kinauzika, kinaendelezwa, kinakuzwa na kubidhaika ulimwenguni kote sambamba na kuwanufaisha watazania kwa ujumla. Baada ya kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa neema na kuwakaribisha waadhimishaji wa MASIKIDU waliotoka katika nchi mbalimbali na watazania kwa ujumla. Aidha, alitoa shukrani za pekee kwa ujumbe uliotolewa kwa Kiswahili safi na fasaha kutoka katika Jamhuri ya Burundi na Msumbiji nchi jirani na nchi ndugu pamoja na ujumbe mrua wa mkurugenzi mkuu wa UNESCO duniani uliosomwa na mwakilishi wake. Alielekeza shukrani na pongezi zake pia kwa Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Mh. Mohamed Mchengerwa na Mh. Mwita Waziri wa Habari, Vijana Utamaduni na Michezo wa Zanzibar pamoja na kamati ya maandalizi na wadau wote wa Kiswahili kwa maandalizi mazuri ya maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani na maandalizi ya wiki nzima katika kuhakikisha maadhimisho hayo yanafana. Pia aliwashukuru watu wote waliojitoa kuadhimisha maadhimisho hayo. Mh. makamu wa raisi alisema kuwa siku hiyo ya tarehe 07 July, 2022 ilikuwa muhimu sana kwa taifa la Tanzania kwani watazania wamepata nafasi ya siku maalumu ya kuadhimisha lugha ya Kiswahili yenye asili ya kifarika ambayo chanzo na kitovu chake ni hapa nchini Tanzania.

Aidha, aliwahakikishia watazania kuwa serikali ya Mh. Samia Hassan iko tayari kushirikiana na taasisi na wadau mbalimbali kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili na kujenga ushawishi wa nchi nyingine kuingiza Kiswahili katika mitaala yao ili kuendelea kusambaza lugha hii adhimu kama ilivyoenezwa katika ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025. Aliwasih watu mbalimbali kuandika vitabu vya kufundishia na kujifunzia lugha ya Kiswahili kwani kuna uhitaji mkubwa wa vitabu hivyo. Hivyo, hatuna budi kukidhi haja hii. Aidha, aliwapongeza wanaotumia vema mitandao ya kijamii na tovuti mbalimbali katika suala zima la kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ulimwengu kwani kwa sasa mitandao ya kijamii na tovuti hizo zina mchango mkubwa sana katika kueneza, kufundisha na kukifanya Kiswahili kuwa sehemu ya maendeleo ya teknolojia, jambo ambalo litachochea kusambaa na kuenea kwa haraka sana kwa lugha ya Kiswahili. Mh. Mpango alisisitiza pia kuwa ili kuendelea kukuza matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili nchini na duniani



hatuna budi kutekeleza maelekezo ya Mh. Raisi Samia aliyoyatoa akiwa makamu wa raisi wakati wa kufungua maadhimisho ya siku ya Kiswahili kitaifa yaliyofanyika tarehe 19-20 Januari, 2021 jijini Dodoma.

Maelekezo yalitotolewa ni pamoja na zana zinazohusika na utamaduni Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni muhimu zibaini maeneo ambayo bado lugha ya Kiswahili hakitumiki ipasavyo ili hatua stahiki zichukuliwe na hususan kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya Kiswahili sanifu na fasaha. Aidha, mabaraza ya Kiswahili yaandae mikakati mahususi ya kukikuza na kukiendeleza Kiswahili ili serikali iyawezeshe kwa kuyapatia wataalamu na kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya miradi ya Kiswahili kwa mabaraza hayo. Kutokana na maelekezo hayo ya Raisi Samia Suluhu Hassan, Mh. Philip Mpango alitoa maelekezo kama ifuatavyo: mosi, wizara na taasisi za serikali ziendeele kutekeleza maagizo ya serikali yaliyokwishakutolewa kwamba nyaraka za mawasiliano za wizara na idara zake ziwe kwa lugha ya Kiswahili, na kwamba mikutano warsha, semina, mijadala ya umma na dhifa zierendeshwe kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, alielekeza kuwa majina ya barabara, mitaa, mabango, fomu za usaili na maelekezo ya matumizi ya dawa zote na bidhaa na huduma pia viandikwe kwa lugha ya Kiswahili. Pili, taarifa za miradi na mikataba inayohusu wananchi ni lazima ziwe kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo, zisiwe kwa lugha ya kigeni. Lengo ni kuwawezesha wananchi kuelewa kila jambo muhimu katika ustawi wa maisha yao.

Tatu, sheria na kanuni ambazo bado hazijatafsiriwa zitafsiriwe na wizara na taasisi zinazosimamia sheria na kanuni hizo kwa kushirikiana na mabaraza ya Kiswahili, wataalamu wengine wa Kiswahili, na ofisi ya mwanasheria mkuu wa serikali. Nne, vyombo vya habari vinavyotumia Kiswahili vihakikishe vinatumia Kiswahili fasaha huku vikizingatia kwa dhati sarufi ya Kiswahili ili pale ambapo anashirikishwa mtu asiyeongea lugha ya Kiswahili chombo cha habari kinachohusika kitoe tafsiri ya maneno yasiyo ya Kiswahili ili wananchi waelewe kinachozungumzwa. Tano, aliagiza balozi zote za Tanzania kuanzisha vituo vya kujifunzia lugha ya Kiswahili. Kwa msisitizo alikazia kuwa, hapa napenda niziagize balozi zote ziwatumie wataalamu wa lugha ya Kiswahili waliosajiliwa kwenye kanzidata ya BAKITA na BAKIZA. Kwa sababu hiyo alitoa maagizo kwa BAKITA na BAKIZA kuchangamkia ombi lililotolewa na Balozi Ishio la kuomba kupatiwa wakalimani wanne mara moja. Aidha, alimtaka Mh. Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Mh. Mohamed Mchengerwa kusimamia suala hilo. Sita, alilitaka Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kushirikiana na BAKIZA kuendelea kuwa wabunifu katika kuzalisha msamiati wa Kiswahili ili kuendana na kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Saba, wizara na taasisi husika, kuhahakisha mfumo wa kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni kwa njia ya mtandao unaoitwa *Swahili Prime* unatumika kikamilifu.

Fursa Alizozibainisha Mh. Philip Mpango

Hotuba ya Mh. Philip Mpango katika maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani, ilibainisha fursa mbalimbali zinazotokana na lugha hii. Katika kuzibainisha fursa hizo, Mh. Mpango alianza kwa kusema kuwa utiaji saine wa hati ya makubaliano ya kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za Afrika ya Kusini na tangazo lililotolewa na serikali ya Uganda la kufundisha Kiswahili kuanzia darasa la kwanza na kuendelea ni fursa muhimu kwa wataanzania. Alisisitiza kuwa sanjari na makubaliano



hayo, mkakati mkuu wa taifa wa kubidhaisha Kiswahili, pamoja na mambo mengine unalenga kuwatangaza wataalamu wetu wa lugha ya Kiswahili katika masoko ya kimataifa na kuitangaza tasnia ya uchapishaji pamoja na kazi za uchapishaji kitaifa na kimataifa.

Mh. Mpango alitoa wito kwa wataalamu wote kushiriki katika kuzitambua na kuzitumia fursa zitokanazo na lugha ya Kiswahili kama kauli mbiu ya maadhimisho ya MASIKIDU inavyoeleza ya kwamba 'Kiswahili kwa Maendeleo na Utangamano wa Dunia'. Kutokana na kaulimbiu hii, Mh. Mpango alisema kuwa hii ni kaulimbiu muhimu sana katika zama hizi ambazo serikali inawahimiza wananchi wake kutafuta fursa zilizoko duniani zitakazowawezesha kupata kipato kupitia lugha ya Kiswahili. Alizitaja fursa hizo kuwa ni pamoja na: shughuli za ukalimani, tafsiri, ufundishaji, uigizaji, uhariri na uandishi wa vitabu. Aidha, lugha ya Kiswahili ni nyenzo muhimu ya kujenga umoja na maelewano, kuwasiliana na kufanya biashara pamoja na utalii. Kutokana na masuala haya muhimu yatokanayo na Kiswahili, Mh. Mpango aliwasiliana wataalamu wa Kiswahili kutumia utaalamu na ubunifu wao kukipeleka Kiswahili huko duniani ili taifa lipate matunda ya ajira na kukuza uchumi wake.

Ushauri na Pongezi za Mh. Philip Mpango kuhusu Lugha ya Kiswahili

Sambamba na kubainisha fursa zinazotokana na Kiswahili, Mh. Philip Mpango aliwashauri pia wapenzi wa lugha ya Kiswahili kuendelea kuongea Kiswahili fasaha na kuandika vitabu vya taaluma mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Aidha, alisema kuwa kwa hali ilivyo sasa, ni dhahiri kuwa tuna uhitaji wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia lugha ya Kiswahili, hivyo hatuna budi kukidhi haja hii. Halikadhalika, aliwapongeza wanaotumia mitandao ya kijamii pamoja na tovuti mbalimbali kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ulimwengu wa sasa. Aliongeza kwa kusema kuwa mitandao ya kijamii pamoja na tovuti hizo vina mchango mkubwa wa kukifanya Kiswahili kuwa sehemu ya maendeleo ya teknolojia jambo ambalo litaifanya lugha ya Kiswahili kusambaa kwa haraka na kwa ufasaha. Sambamba na ushauri huo Mh. Mpango alionesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili. Akinukuu shairi la mtunzi wa mashairi ya lugha ya Kiswahili Shaaban Robert lisemalo: 'Titi la Mama litamu' lililochapishwa katika kitabu chake cha mkusanyiko wa mashairi cha 'Pambo la Lugha' alisema:



‘Titi la mama litamu, hata likiwa la mbwa,
Kiswahili naazimu, sifayo iliyofumbwa,
Kwa wasiokufahamu, niimbe ilivyo kubwa,
Toka kama mlizamu, funika palipozibwa,
Titile mama litamu, jingine haliishi hamu’.

Kutokana na shairi hili, Mh. Philip Mpango alisema ya kwamba mwandishi Shaaban Robert anaulinganisha utamu wa lugha yetu adhimu na aushi ya Kiswahili na titi la mama kwa mtoto wake. Anaendelea kudadavua kuwa ni imani yake kwamba kila mtu anaamini kuwa lugha yetu ya Kiswahili ni tamu kama titi la mama lilivyo kwa mtoto. Hivyo, ni wajibu wa kila mmoja kuendelea kuenzi lugha hii kwa kuendeleza matumizi yake sahihi na kuonesha umuhimu wake kwa wasioifahamu hata waone hamu ya kuitumia kama alivyoandika Shaaban Robert. Halikadhalika, alitoa shukrani za dhati kwa washairi nguli kama vile Saadan Abdulkandoro, Mohamed Asefu Atibu, Shee Karuta Amil Abeid, Profesa Kezilahabi na wengine kwa mchango wao wa kueneza Kiswahili.

Wengine aliowashukuru ni pamoja na Mzee Ali Hassan Mwinyi raisi mstaafu wa Tanzania wa awamu ya pili, walimu wote wa shule za msingi na sekondari, wahadhiri wa vyuo vikuu kwa kufundisha lugha ya Kiswahili. Vilevile aliwahimiza vijana kuwa na tabia ya kusoma na kuandika vitabu vya Kiswahili na kuwa mstari wa mbele kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Aliendelea kuisitiza kuwa tunataka kuwa na akina Shaaban Robert, Mohamed Seif Atibu na Mzee Shafi Adam Shafi wengi zaidi ambao watasomwa vizazi na vizazi duniani. Kutokana na maazimio, matamko na ushauri huo, ni wazi kwamba Makamu wa raisi, Mh. Philip Mpango ana mchango mkubwa katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili katika karne hii ya 21. Halikadhalika, watanzania miongoni mwa masuala kadhaa tulioshauriwa, tumesisitizwa kuchangamkia fursa zinazotokana na Kiswahili, hivyo, tusiziache zichukuliwe na watu wa mataifa mengine tu. Viongozi wengine walikuwa bega kwa bega na viongozi waliotangulia kwa kutoa mchango wao kama inavyojadiliwa hapa chini:

Maazimio Yaliyotolewa na Mh. Waziri Adolph Mkenda

Waziri Adolph Mkenda ni Waziri wa Elimu katika awamu ya sita ya uongozi nchini Tanzania. Waziri Mkenda alianza hotuba yake kwa kusema kuwa: ‘Leo 07 Julai, 2022 tunaingia makubaliano rasmi na Afrika Kusini kushirikiana katika mambo mbalimbali ya elimu ya msingi mathalani, kufundisha Kiswahili nchini humo’. Kutokana na kauli hiyo alisema kuwa kusaini ni jambo moja na kutekeleza ni jambo jingine. Hivyo, kuna mkakati wa kuandaa mpangokazi na kualika timu za ufundi kutoka Afrika Kusini kuja Tanzania na kukutana na timu ya hapa Tanzania inayoongozwa na katibu mkuu Frances Michael kwa ajili ya kujadili namna ya kutekeleza suala hilo. Aliongeza kwa kusema kuwa baada ya hapo watafanya ziara ya kwenda Afrika Kusini kwenda kushuhudia mkakati wa kuweka saini kwenye mpangokazi wa utekelezaji kama ilivyoelekezwa na raisi ili isiwe tu makubaliano ya kusaini na kuyaweka kabatini. Alisistiza kuwa serikali itashirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo ambayo ndiyo iliyoandaa maadhimisho hayo. Pia watashirikiana na serikali ya mapinduzi ya Zanzibar na Waziri kutoka Afrika Kusini kuhakikisha kuwa yote hayo



yanatekelezwa. Baada ya kuyasema hayo, aliongeza kuwa, Tanzania ndicho kitovu, chimbuko na vinara wa Kiswahili fasaha. Hivyo, tuna wajibu wa kukuza, kutunza na kueneza Kiswahili fasaha. Alimalizia kwa kufafanua kuwa haitapendeza kwenda kufundisha Kiswahili duniani kama sisi wenyewe tunaboronga Kiswahili chetu. Kwa hiyo, tujitahidi kuzungumza Kiswahili fasaha kwa kukuza lahaja rasmi iliyotumika kukisanifisha Kiswahili. Sambamba na matamko na maazimio ya Mh. Adolph Mkenda, pia Mh. Mohamed Mchengerwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo alitoa maazimio na matamko kadhaa kuhusiana na lugha ya Kiswahili:

Maazimio, Matamko na Ushauri wa Mh. Mohamed Mchengerwa

Mh. Mohamed Mchengerwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo alianza kwa kumshukuru Mh. Samia Suluhu Hassan Raisi wa Tanzania kwa kufanikisha maadhimisho hayo. Pia aliwashukuru wazee mathalani, Mzee Abdulrahman Kinana makamu mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara na wote walioambatana naye kwa kuisherehesha MASIKIDU. Aidha, aliwashukuru kwa kutoa machozi na kuvuja jasho katika harakati za kuhakikisha watanzania wanaungana kwa pamoja kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Aliongeza kwa kusema kuwa, tunakili kabisa kwamba tumepiga hatua na kama taifa lazima tujipongeze kwa jitihada na kazi kubwa ambayo imefanywa na waasisi wa taifa hili hadi kufikia hapa tulipofika. Kutokana na hayo alisema kwamba Kiswahili kimetabiriwa kuwaunganisha watu wote duniani kwa kuwa ni mojawapo ya lugha itakayotumika katika mikutano mbalimbali ya kimataifa. Kwamba, Kiswahili kimekuwa ni lugha ya kutuunganisha na kutufanya watanzania tuwe wamoja. Hivyo, aliwashauri watanzania kuendeleza mshikamano baina yao bila kujali itikadi na ukanda wao.

Halikadhalika, alishauri kuwa pamoja na kwamba tunakipigania Kiswahili tusikiache kabisa ili tuweze kuingia katika ushindani wa dunia. Alisema pia kuwa kama taifa kuna mambo ya msingi ila hatuyaoni kuwa yana msingi na ndiyo maana tunapitwa na mambo mengi muhimu. Aliongeza kuwa tumekuwa ni watu ambao hatupendi kuongeza uweledi na ufahamu. Ili kuthibitisha usemi huo, alimrejelea msemaji kutoka Kenya Mzee Wallah Bin Wallah aliyesema kuwa, “watanzania mko kwenye kisima cha maji (Kiswahili) mnaogelea humo ila cha kushangaza mnaomba maji hayohayo kwa wale wanaochota maji hayo kwa kata” Kutokana na maneno hayo Waziri Mchengerwa alifafanua kuwa Kiswahili kimezaliwa Tanzania lakini wakenya wananufaika nacho sana. Alitoa rai kwa kuiagiza BAKITA kuhakikisha kwamba wanatumia fursa ambazo zinatokana na Kiswahili ambacho kimezaliwa hapahapa Tanzania. Katika hoja hii alithibitisha kuwa ipo changamoto ya wenzetu wakenya kuchangamkia fursa hizo zaidi ya watanzania. Aidha, alimuomba kila mtanzania kuthubutu kutumia fursa mbalimbali zinazotokana na lugha ya Kiswahili. Aliongeza kwa kusema kuwa tunataka sisi watanzania kuwa namba moja kwa kila jambo.

Mh. Mchengerwa alitamka kuwa inawezekana kila mtanzania kuongeza weledi, kujituma, kupunguza uvivu na kuongeza ufahamu. Waziri Mchengerwa alisisitiza kuwa jambo hili linawezekana kwani sisi watanzania ndiyo tumewafundisha Kiswahili watu wa mataifa mengine kwani wengi huja Tanzania kijufunza lugha hii. Kwa mfano, wakenya, waganda, nakadhalika. Lakini jambo la kushangaza haohao tuliowafundisha ndiyo wamekuwa walimu katika vyuo vikuu mbalimbali duniani, watafsiri katika mikutano mbalimbali mikubwa ya kimataifa. Mh. alisema



kwamba inawezekana tukaonekana ni wazungumzaji wazuri wa Kiswahili lakini wenzetu wa mataifa mengine wakawa wamepiga hatua kwa kutafsiri, kufundisha na kuonekana wao ni mahiri zaidi katika Kiswahili wakati sisi watanzania tumelala na hatuko kwenye Kiswahili wala Kiingereza. Hivyo, watanzania tuna kazi kubwa ya kukipigania Kiswahili. Waziri Mchengerwa aliwaamuru BAKITA kuipatia wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo kanzidata (data base) ya wataalamu wa Kiswahili kuanzia wasiokuwa na shahada, wenye shahada ya kwanza, ya pili na ya tatu. Lengo la kanzidata hiyo kwa maelezo yake ni kuona namna ya kuchangamkia fursa zinazopatikana katika Kiswahili kwani bila ya kuwa na kanzidata hawataweza kutambua wataalamu wa Kiswahili waliomo nchini Tanzania.

Aliendelea kusema kuwa ni lazima kujivunia lugha yetu ya Kiswahili pale tunapokwenda kwenye matamasha mbalimbali, na pale viongozi wetu wanapokwenda kwenye mataifa mengine watoe kamusi zetu kama tuzo kwa kuzigawa kwenye mataifa mbalimbali ili mataifa hayo yajue kabisa kuwa msingi wa Kiswahili ni Tanzania. Aidha, aliisihi BAKITA kuwa ina kazi kubwa ya kufanya ili kukibidhaisha Kiswahili. Waziri Mchengerwa aliwaonya BAKITA kuwa kama walikuwa wanakaa tu ofisini, sasa ndiyo wakati wa kujipanga kwelikweli ili Kiswahili kibidhaishwe nje ya Tanzania. Aliwasihii watanzania kujidhatiti kwelikweli vinginevyo dhana ya kubidhaisha Kiswahili itakwama na badala yake itabaki kuwa lugha ya kuandikwa kwenye magazeti na kusomwa tu na haitakuwa na faida kwa taifa letu.

Alisema kuwa wizara yake imelipokea ombi la Kiswahili kutumika katika elimu ya Tanzania ambapo alitamka kuwa kumekuwa na mjadala mkubwa sana ndani ya bunge juu ya suala hilo. Hivyo, kwa kushirikiana na bunge, na wizara ya elimu watabadilishana mawazo na kuona ni hatua gani ambayo itachukuliwa na serikali. Halikadhalika, alitamka kuwa wao kama serikali tayari wameandaa mpangomkakati wa kubidhaisha Kiswahili ndani na nje ya Tanzania. Mpangomkakati huo kwa maelezo yake unalenga kubaini mambo yafuatayo: mosi, kuhakikisha kuwa BAKITA wanaandaa kanzidata ya wataalamu wa Kiswahili na maeneo yao ya utaalamu. Pili, kuwapatia watanzania elimu ya namna ya kutafuta fursa za Kiswahili ambazo mataifa mengine wameishaanza kuzichangamkia. Tatu, kuwaunganisha watanzania na fursa za Kiswahili na kuhakikisha kuwa wanatumia fursa nyingi za Kiswahili zilizo duniani. Alitamka kuwa huu ni mkakati wa miaka kumi ambao unaanzia 2022 hadi 2032 na kuwa utazinduliwa siku ya 07 Julai, 2022 siku ya kilele cha MASIKIDU. Baada ya kuona mchango wa Mh. Mchengerwa katika harakati za kukikuza na kukieneza Kiswahili, tuone mchango wa viongozi wengine:

Maazimio, Matamko na Ushauri wa Mh. Abdulrhaman Kinana

Kiongozi huyu alianza hotuba yake kwa kuelezea kazi ya lugha ya Kiswahili kwa ujumla. Alieleza kuwa Kiswahili tunachokizungumza leo hii kinaendelea kukua kila siku na kila siku tunapata maneno mapya na nahau mpya zinazokikuza na kukiendeleza Kiswahili. Alieleza kazi ya Kiswahili kuwa ni pamoja na kuikomboa Tanzania. Kwamba ukombozi wa Tanzania umeanza miaka mingi sana. Ukombozi rasmi wa mapambano ya kisiasa ulianza 1954 chama cha TANU kilipozaliwa. Yalipendekezwa na yakaendelezwa mapambano ya kisiasa ambayo hayakuwa ya umwagaji damu. Aliendelea kusema kuwa katika kipindi kifupi sana cha miaka saba tukawa tumepata uhuru wa nchi



yetu (Tanganyika kipindi hicho) tofauti na nchi nyingine. Alifafanua kuwa moja ya chombo kilichosaidia ukombozi wa Tanzania na kupatikana kwa uhuru mapema ni mchango wa lugha ya Kiswahili katika shughuli nzima ya ukombozi. Kwa sababu watu wote walikuwa wanazungumza Kiswahili, viongozi na wananchi walikuwa wakiwasiliana kwa kutumia lugha ya Kiswahili, mikutano ya hadhara ilifanyika kwa lugha ya Kiswahili na ujumbe kupitia vituo vya redio uliwafikia wahusika kwa kutumia lugha hiyo. Hivyo, Kiswahili kilirahisisha mawasiliano na kutoa mchango mkubwa sana katika kuharakisha ukombozi wa taifa letu. Alifafanua pia kuwa baba wa taifa na viongozi wenzake wa Chama cha TANU wakati ule walizunguka nchi nzima, mikoa kwa mikoa, wilaya kwa wilaya, vijiji kwa vijiji kuzungumza na watanzania juu ya harakati za ukombozi wa nchi yetu, harakati za kutafuta uhuru. Kupitia Kiswahili, watanzania waliwaelewa viongozi hao kwa haraka na tukaweza kupata uhuru mapema sana. Kwa hiyo, Kiswahili ni lugha iliyosaidia sana katika suala zima la ukombozi wa Bara la Afrika. Hata baada ya uhuru Kiswahili kilitusaidia sana kujenga umoja wa kitaifa wa nchi yetu.

Umoja wa nchi yetu tuliyonao umetokana na lugha ya Kiswahili. Aidha, lugha hii imesaidia ukombozi wa Kusini mwa Afrika ambapo ziko baadhi ya nchi za Kusini mwa Afrika ambazo sehemu yake ndogo sana ya wananchi wake wanazungumza Kiswahili. Kwa mfano, raia wengi wa Msumbiji hawazungumzi Kiswahili lakini raia wengi wanaoishi Kaskazini mwa Msumbiji wanazungumza Kiswahili. Na huko ndiko zilikoanzia harakati za ukombozi. Mathalani, katika jimbo la Quelimane ambalo liko mpakani na Tanzania. Hivyo, ilikuwa rahisi kutumia lugha ya Kiswahili kuanzisha ukombozi kwa baadhi ya nchi Kusini mwa Afrika. Si hivyo tu, bali hata nchi ambazo zilikombolewa Kusini mwa Afrika, chombo kikuu kilichosaidia ukombozi wa nchi hizo ni majeshi yao. Mathalani, majeshi ya Namibia na majeshi ya nchi mbalimbali yalisaidia kuleta ukombozi wa nchi zao. Majeshi hayo yalifanya mafunzo kwa Kiswahili suala lililosaidia sana katika kujifunzia matumizi ya siraha, mbinu za kivita, mikakati na lugha ya kuwasiliana miongoni mwao. Hii ni kutokana na sababu kuwa wanajeshi walitoka nchi mbalimbali na wakaamua kutumia lugha ya Kiswahili kama njia kuu ya mawasiliano. Hivyo, Kiswahili ikawa ndiyo lugha ya kimapigano.

Aliendelea kuelezea kuwa katika mapambano ya aina hii lazima kuwe na umoja na maelewano vinginevyo wanaweza kupishana. Aidha, jeshi la Uganda wakati huo ikiongozwa na raisi Mseven, walitumia Kiswahili kuliandaa jeshi lao na kuandaa harakati za mapigano katika harakati za kumuondoa Nduli Idd Amini madarakati. Halikadhalika, kwenye sherehe za kijeshi za Uganda, amri za kijeshi na mafunzo ya kijeshi pia hutolewa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, tunaposema lugha ya Kiswahili ni lugha ya ukombozi ipo mifano dhahiri na tafsiri inayolidhihirisha hili. Mh. Abdulrahman Kinana alitoa mfano pia wa Rwanda kwamba raisi Kagame na majeshi yake katika kuondoa udhalimu uliokuwepo katika nchi yao wakati ule, majeshi yao yaliendesha mafunzo kwa kutumia lugha ya Kiswahili, yaliendesha mapambano kwa lugha ya Kiswahili vilevile. Hadi leo wanaongoza katika kuzungumza na kukuza lugha ya Kiswahili katika nchi hizi za Uganda na Rwanda ni wanajeshi ambao walikitumia Kiswahili kama lugha ya mafunzo na mapigano ya kivita. Hii ndiyo maana rais Mseven na raisi Kagame wanazungumza Kiswahili vizuri kwa sababu



waliongoza mapambano kwa kutumia lugha hii. na wao wenyewe waliendelea kukuza lugha hii. Aidha, alitamka kuwa serikali ya Uganda imeamua kuwa Kiswahili kiwe lugha rasmi katika nchi yao.

Mh. Abdulrahman Kinana alieleza pia kuwa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kulikuwa na mapambano ya kumuondoa Marshal Mobutu na kuingia madarakani kwa Mzee Joseph Kabila. Kutokana na hilo, majeshi yake yalianza kutokea nchi za maziwa makuu mpaka yakafikia Kinshasa. Majeshi yale yote yaliandaliwa na kufanya mafunzo ya kijeshi, yakapambana hadi wakasherekea jitihada zao na ushindi kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hadi leo Kiswahili kinazungumzwa katika maeneo hayo ikiwa ni pamoja na nchi za DRC japokuwa Kiswahili chao si kizuri sana lakini kinazungumzwa na wahusika wanaelewana hasa Mashariki mwa Kongo. Aidha, raisi Kabila na viongozi wengine wengi ni wazungumzaji wazuri wa Kiswahili. Hivyo, Kiswahili imekuwa nyenzo kubwa ya ukombozi Kusini mwa Afrika.

Alifafanua kuwa ilevile wapo viongozi na wananchi ambao hawakuwa mabingwa wa lugha ya Kiswahili, lakini ilipozungumzwa lugha hii walielewa. Kwa mfano, Raisi Samola Mashehe, hakuzungumza Kiswahili vizuri sana lakini kikizungumzwa alielewa sana. Mara kadhaa alipendelea kuzungumza Kireno kuliko Kiswahili lakini endapo Kiswahili kingezungumzwa ndivyo sivo, alikuwa anaelewa na kugundua makosa yaliyofanyika. Kwa maana hiyo, Kiswahili kimesaidia kujenga umoja miongoni mwa wapiganaji. Hakuna ufanisi katika mapigano pasipokuwa na umoja, mkiwa na umoja mtasonga mbele kwa uhakika. Mh. Abdulrahman Kinana alitoa mifano ya msamiati wa Kiswahili uliotumika katika mapigano ya kivita kuwa ni kama vile: kaa chini, simama juu, piga mzinga nakadhalika. Hata baada ya ukombozi lugha hii ilitusaidia sana kujenga ujirani mwema miongoni mwa nchi zetu. Alisema kuwa ana uhakika kuwa Tanzania na nchi zinazozungumza Kiswahili mathalani, Tanzania na Kenya, Tanzania na Uganda, tuko karibu zaidi kuliko zile nchi ambazo hazizungumzi Kiswahili. Ikumbukwe kuwa mwaka 1966 tuliunda Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiongozwa na Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Jomo Kenyata. Mojawapo ya jambo lililotufanya kuungana ni kwamba sote tulikuwa tunaongea lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, misingi ya umoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imejengwa katika lugha ya Kiswahili. Hata leo bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki na jumuiya yenyewe katika shughuli mbalimbali, matumizi ya Kiswahili yanatambuliwa kama lugha rasmi ya kuendesha shughuli hizo. Hivyo, lugha hii imetusaidia kujenga ujirani mwema.

Aidha, lugha ya Kiswahili imevuka mipaka kutoka lugha ya kuleta ukombozi wa nchi zetu na kuwa lugha ya ukombozi wa kiuchumi, lugha ya kujenga umoja miongoni mwa nchi zetu. Haya yalikuwa maelezo ya Mh. Kinana. Mbali na hayo, aliongeza kwa kusema kuwa pia Kiswahili kinatumiwa na maraisi pale wanapokuwa katika Jumuiya ya Nchi za Afrika (AU), huhutubia kwa lugha ya Kiswahili na lugha hii inakubalika kuwa ndiyo lugha rasmi ya matumizi katika Umoja wa Nchi Huru za Afrika. Vilevile shirika la Elimu na Sayansi la Umoja wa Mataifa nalo limetambua Kiswahili kama lugha maalumu. Mh. Abdulrahman Kinana alisema kuwa sisi watanzania ndiyo kitovu cha lugha hii lakini kwa bahati mbaya siyo wafaidikaji wakuu wa Kiswahili, wafaidikaji ni watu wengine na siyo watanzania. Kwa mfano, Kiswahili kinazungumzwa rasmi katika nchi kama 18 hivi na mapato



yanayotokana na matumizi ya lugha ya Kiswahili duniani ni dola million moja na laki tatu (milioni 1.3). Mapato hayo yanatokana na wanafunzi, wakufunzi, wakalimani, redio na televisheni zinazozungumza idhaa ya Kiswahili.

Fursa Alizozibainisha Mh. Abdulrahman Kinana

La kujiuliza hapa ni kwamba katika hizo dola moja na laki tatu sisi watanzania tunanufaikaje? Tuna watu wangapi duniani wanaofundisha lugha ya Kiswahili na wanakwenda kutangaza lugha hii? Mh. alisema kuwa haoni haya kusema kuwa walimu wengi wanaofundisha Kiswahili duniani hawatoki Tanzania. Aidha, nchi inayoongoza katika suala hilo ni Kenya. Ukitazama duniani ziko nchi 72 zenye taasisi zinazofundisha lugha ya Kiswahili. Marekani pekee ina taasisi za elimu ya juu 112 zinazofundisha Kiswahili, China inazo 3. Je, ni watanzania wangapi wanaofundisha katika taasisi hizo? Aidha, aliuliza kuwa je, ni watanzania wangapi wanafundisha Kiswahili katika vyuo vikuu maarufu duniani vunavyofundisha Kiswahili kama vile Harvard, Stanford nakadhalika.

Mh. Kinana alitamka kuwa wakalimani wa kitanzania wanaotafsiri lugha mbalimbali kama vile Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kireno katika Kiswahili na kinyume chake (Kiswahili kwenda lugha hizo), duniani hawazidi hata 80. Alisema kuwa kwa hakika hii ni fursa ya kuchangamkia kwani watanzania tuko milioni sita na wanaokieneza Kiswahili duniani ni wachache mno. Aliongeza kuwa zipo redio 183 na TV 38 duniani zinazotumia lugha ya Kiswahili, hapa Tanzania zipo redio 183 na TV 38 pia. Anashauri kuwa vituo hivi vya redio na TV ni fursa muhimu kwa watanzania kukuza na kukinadi Kiswahili na kukifanya kuwa lugha ya biashara na kipato. Kwa kuisitiza jambo hili alisema kuwa hana shaka na serikali inayoongozwa na Mh. Raisi Samia Suluhu Hassan na wizara yake ya Utamaduni inayoongozwa na Waziri Mohamed Mchengerwa na watendaji wake kwa namna wanavyokwenda mchakamchaka kuhusiana na lugha hii adhimu ya Kiswahili. Hivyo, Tanzania itakuwa na fursa nyingi sana. Aidha, alimshukuru Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere kwa kukuza Kiswahili kwa njia ya utunzi wa vitabu vya lugha ya Kiswahili na kutafsiri vitabu mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili kikiwemo kitabu cha Mabepari wa Venisi. Sambamba na hilo, alimshukuru kwa kutumia lugha ya Kiswahili kati yake na wananchi aliokuwa akiwaongoza, kueleweka vizuri pale alipozungumza kwa lugha ya Kiswahili hata kama ni dakika chache au kwa muda mrefu, kila mtu alifurahi na kutaka kuendelea kumsikiliza muda wote. Mh. Kinana alizidi kuisitiza kuwa Mwl. Julius Kambarage Nyerere alitumia mikutano ya hadhara kuhutubia, kuburudisha, kufurahisha na kueleimisha umma, hakika alikuwa kiongozi mahiri sana na alitoa mchango mkubwa sana. Pamoja na hayo, alikuwa pia kiongozi, mwanaharakati mwanamikakati wa ukombozi siyo kusini tu mwa Afrika bali pia Bara lote la Afrika. Alitaja baadhi ya nchi alizokomboa Mwl. Nyerere kutoka mikononi mwa wakoloni kuwa ni pamoja na nchi za Kusini mwa Afrika mathalani, Afrika Kusini, Mozambiq, Namibia na Zimbabwe. Pia alitaja nchi nyingine kuwa ni Guinea Bissau, Vietnam nakadhalika.

Hitimisho

Suala la kutekeleza makubaliano miongoni mwa wahusika huwa ni gumu kiasi cha kuwafanya kuishia tu kukubaliana bila ya kuwa na utekelezaji juu ya yale waliyokubaliana. Aidha, maazimio, matamko na ushauri hutolewa kwa urahisi lakini utekelezaji wake huwa na ukakasi kama asemavyo



Hans (2016) alipotafiti kuhusu tathmini ya matamko yaliyoainishwa katika waraka wa serikali uliotolewa na aliyekuwa waziri wa Habari Utamaduni na Michezo Mh. Mkuchika wa mwezi Aprili, 2010 kuwa pamoja na maelekezo yaliyotolewa na viongozi waandamizi wa serikali ya Tanzania kuhusu matumizi ya Kiswahili bado kuna semina na warsha nyingi zinaendeshwa kwa lugha ya Kiingereza. Aliongeza kuwa jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba hata ripoti za warsha hizo huandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Maazimio, matamko na ushauri uliotolewa na viongozi mbalimbali katika MASIKIDU kuhusu lugha ya Kiswahili ni ya msingi, yamegusia nyanja mbalimbali na yanalenga kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili katika karne hii ya 21. Mtafiti anatoa rai kwa serikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Mh. Samia Suluu Hassan Raisi wa Tanzania, kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa maazimio, matamko na ushauri huo. Aidha, mtafiti wa makala hii anawasihi wataanzania kutoka usingizini na kuchangamkia fursa mbalimbali zinazotokana na Kiswahili, mathalani, uandishi wa vitabu vya mbalimbali vya Kiswahili vikiwemo vya kufundishia na kujifunzia, tafsiri, ukalimani, ufundishaji wa lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania nakadhalika. Ushauri umetolewa kwa BAKITA na BAKIZA kuendelea kuwa wabunifu katika kuzalisha msamiati wa Kiswahili ili kuendana na kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia, kutumia fursa zinazotokana na Kiswahili. Vilevile imeshauriwa, BAKITA kuipatia wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo kanzidata ya wataalamu wa Kiswahili kuanzia wasiokuwa na shahada, wenye shahada ya kwanza, ya pili na ya tatu na kubidhaisha Kiswahili ndani na nje ya Tanzania. Ni matumaini yetu kuwa mabaraza haya yatatekeleza maagizo na ushauri huo ili kukikuza na kukieneza Kiswahili ulimwenguni kote. Mtafiti ameonesha raghba yake ya kukipenda, kukikuza na kukieneza Kiswahili, na hivyo kuhimiza suala la kubidhaisha, kuimarisha matumizi yake ndani na nje ya Tanzania sambamba na kutumia fursa zinazotokana na lugha hii aushi ya Kiswahili. Mtafiti amejikita katika maazimio, matamko na ushauri uliotolewa na viongozi wa serikali ya Tanzania. Tunatambua kuwa pamoja na maazimio, matamko na ushauri tulioubainisha katika makala hii ni muhimu mno katika kukieneza na kukiendeleza Kiswahili. Kadhalika, wapo viongozi kadhaa na waswahili wenye mapenzi mema na lugha ya Kiswahili waliotoa maazimio, matamko na ushauri kwenye MASIKIDU. Vilevile zipo shughuli zilizoendeshwa kwenye juma zima la maadhimisho hayo zilizolenga kukikuza na kukieneza Kiswahili. Hivyo, utafiti mwingine unaweza kushughulikia maeneo hayo.

Marejeleo

- Gibe, A. G. (1983). Tanzania's Language Policy with Special Reference to Kiswahili as an Educational Medium: Katika *Kiswahili*. Juz. 50 Na. 1. Uk. 46-50.
- Hans, M. (2016). Tathmini ya Utekelezaji wa Matamko ya Viongozi Waandamizi wa Serikali ya Tanzania kuhusu Matumizi ya Kiswahili. katika *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istitlahi*, Dar es Salaam, Daud Publishing Company Limited. Tanzania. uk. 2-18.
- Kimathi, M. na Mukuthuria, M. (2017). "Lugha na Utandawazi: Nafasi ya Kiswahili katika Kukuza na Kuendeleza Demokrasia Nchini Kenya". Katika *Mwanga wa Lugha*, Juz. 1 na 2. Uk. 27-42.
- Massamba, D. P. B. (2007). *Kiswahili Origins and Bantu Divergence-Convergence Theory*, TUKI Dar es Salaam.



- Msanjila, Y. P. (2005). "Problems of Writing in Kiswahili: A Case Study Kigurunyembe and Morogoro Secondary Schools in Tanzania". *Nordic Journal of African Studies*. Vol. 14(1). Uk.15-25.
- Mulokozi, M. M. (1992). "A Survey of Kiswahili Literature". 1970-1988. *Katika Africa Focus*. Juz. 8 Na. 1. Uk. 49-61.
- Mutembei, A. (2011). "Kukitandawazisha Kiswahili kupitia Simu za Kiganjani: Tafakari kuhusu Isimujamii". *Katika Swahili Forum*, Juz. 18: Uk. 198-210.
- Mutembei, A. (2016). "Utandawazi wa Lugha za Kiafrika: Nafasi ya Kiswahili Sanifu katika Afrika Inayobadilika". *Katika Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*, Dar es Salaam, Daud Publishing Company Limited. Tanzania. Uk. 453-476.
- Mwansoko, H. J. M. (2016). "Ukuzaji wa Kiswahili Kupitia Tafsiri: Hatua Moja Mbele, Mbili Nyuma", *katika Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*, Dar es Salaam, Daud Publishing Company Limited. Tanzania. Uk. 2-18.
- Sharifu, I. N. (1988). *Tungo Zetu; Msingi wa Mashairi na Tungo Nyinginezo*. Trenton: The Red Sea Press Inc.
- Mazrui, A. M na Shariff, I. N. (1994). *The Swahili: Idiom and Identity of An African People*. Trenton: Africa Word Press.
- Mazrui, A. M na Alamin, M. (1998). *The Power of Babel: Language and Governance in the African Experience*. Chicago: University of Chicago Press.